# Mapitio ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999

*Y. A. B. Mkinga*

**Harakati za Mwanzo**

Mwezi Julai 1991 Baraza la Sanaa la Taifa liliunda Kamati ya watu tisa (9) ambayo ilipewa hadidu za rejea nne:

(i) Kupitia na kuichunguza sheria ya Hakimiliki Na. 61 ya 1966;

(ii) Kutuma mapendekezo rasmi kwa BASATA ya kuiboresha sheria hiyo;

(iii) Kuwahamasisha watunzi na wasanii watoe maoni na mapendekezo yao ya sheria muafaka ya masuala ya hakimiliki na hakishiriki;

(iv) Kuanzisha majadiliano ya masuala ya ulinzi wa hakimiliki na hakishiriki kwenye magazeti, redio, luninga, vyuoni n.k.

Kamati hiyo iliwasilisha ripoti yake BASATA mwezi Mei, 1992.

Maendekezo muhimu yalikuwa:

a) Waraka wa Baraza la Mawaziri uandaliwe ukipendekeza sheria Na. 61 ya 1966 ifutwe na sheria muafaka iandaliwe.
b) Serikali, ikishirikisha kikamilifu wadau wa hakimiliki na hakishiriki na kwa msaada wa WIPO, iandae rasimu ya sheria hiyo mpya.

Mwezi Septemba, 1997 Baraza la Mawaziri lilipitisha Waraka uliopendekeza sheria mpya itayarishwe. Ndipo mwezi Aprili, 1999 Wizara ya Sheria, ikishirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, iliwasilisha muswada Bungeni. Bunge lilikubali kwa kauli moja. Tarehe 2 Juni, 1999 Mheshimiwa Rais aliikubali sheria hii.

Tarehe 31 Desemba, 1999 ni siku iliyoteuliwa na Waziri wa Viwanda na Biashara ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

## Mapitio ya Vipengele vya Sheria

### Utangulizi

Kutunga sheria ya hakimiliki na hakishiriki ili kukuza viwango vya wabunifu wa kazi za sanaa, kuhifadhi mambo ya vitu vya kale na kulinda haki za kiuchumi za wasanii, watayarishaji wa kanda, watangazaji, mambo ya vitu vya jadi na mengineyo.

Sheria hii imegawanywa katika sehemu saba:

Sehemu I: (Vifungu 1-4): mambo ya utangulizi: jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, eneo ambalo sheria itatumika, madhumuni na ufafanuzi wa maneno (definitions).

Sehemu II: (Vifungu 5-23): vinashughulikia masuala ya ubunifu (utunzi na sanaa) ambazo zinastahili zilindwe.

Sehemu III: (Vifungu 24-30): vinahusu ulinzi wa mambo ya vitu vya jadi/utamaduni (expressions of folklore).

Sehemu IV: (Vifungu 31-35): ulinzi wa wasanii (performers), watayarishaji wa kanda na watangazaji wa habari.

Sehemu V: (Vifungu 36-41): makosa ya madai na ya jinai ya ukiukwaji (infringement) na adhabu zake.

Sehemu VI: (Vifungu 44-51): ukiukwaji wa kiteknolojia wa hakimiliki/shiriki, urekebishaji wa adhabu zake.

Sehemu VII: (Vifungu 52-53): masharti ya mambo ya mpito.

**Sehemu I: Madhumuni**

Kifungu cha 2 kinaeleza kuwa madhumuni ya sheria ni kukuza viwango vya ubunifu wa kazi za sanaa, kuhifadhi mambo ya vitu vya jadi, kulinda haki za kiuchumi za msanii, watayarishaji wa kanda na watangazaji wa habari.

Kifungu 3(1) kinasema sheria hii inahusu:

(a) kazi za watunzi/wasanii ambao ni raia wa, au wanaishi, nchini Tanzania

(b) kazi ambazo zilichapishwa kwanza nchini, licha ya uraia wa mtunzi

(c) kanda za sinema zilizotayarishwa na mkazi wa hapa

(d) kazi za uhandisi majengo (architecture) nchini.

Hata hivyo ikumbukwe kuwa Sheria hii haitumiki na haitambuliki na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kuwa suala hili si la Muungano.

Kifungu cha 4 kinatoa ufafanuzi wa maneno mbalimbali kama vile "Mambo ya vitu vya jadi", Hakishiriki" na Taarifa za kusimamia haki"(RMI).

**Sehemu II: Hakimiliki**

Kifungu 5(1) kinatamka kuwa watunzi wa kazi asili za sanaa wana haki ya ulinzi -- bila kufuata taratibu nyingine zozote kama. usajili.

Kifungu 5(2) kinaelezea kazi za utunzi na sanaa ambazo zinajumuisha:

(a) vitabu, makala, maandishi mengine, pamoja na michoro ya kompyuta
(b) hotuba, mahubiri
(c) kazi za drama
(d) kazi muziki
(e) michezo/mitindo ya muziki
(f) mikanda ya sinema
(g) michoro, uhandisi majengo picha (foto)
(h) kazi za mikono (ufinyanzi, vikapu, vinyago)
(i) ramani, michoro (skechi)

Kazi zote hizi zinalindwa bila kujali namna zilivyoelezwa, hadhi na madhumuni ya kuanzishwa.

Pia, kazi zinazotokana (derivative) na kazi asili k.m. tafsiri, fupisho, muunganisho (encyclopaedia) n.k. zinatambuliwa na kulindwa kama kazi asili.

**Haki za Kiuchumi za Kazi za Utunzi na Sanaa**

Chini ya kifungu cha 9 mtunzi na msanii ana haki za kiuchumi zifuatazo:

(a) haki za kutengeneza nakala/kudurufu
(b) haki za kuzisambaza
(c) haki za kukodisha nakala halisi za kanda, filamu na michoro ya kompyuta
(d) kuzitangaza kazi hizo (exhibit)
(e) haki za kuzitafsiri
(f) haki za kuzibadili (adapt)
(g) haki za kuzicheza mbele ya umma
(h) haki za kuzitangaza kwenye redio au televisheni
(i) haki nyingine za kuziwasilisha kwa umma
(j) haki ya kuingiza nakala nchini (importation).

- kibali cha pekee au cha ujumla
- eneo la leseni
- muda wa leseni
- leseni iwe kimaandishi
- mauzo ya kibali (kwa ridhaa ya mtunzi) n.k.

**Sehemu III: Ulinzi wa Mambo ya Vitu vya Jadi**

Kifungu 23: "vitu vya jadi" vinajumuisha:

(a) hadithi za jadi, tungo za kiushauri na vitendawili
(b) nyimbo za utamaduni na ala za jadi
(c) ngoma za utamaduni, michezo ya kuigiza na mambo ya matambiko
(d) michoro, picha, vinyago, kazi za ufinyanzi, uhunzi wa chuma, vipuri, vikapu, mavazi
(e) vyombo vya muziki vya utamaduni.

Kifungu 25: kinaweka masharti ya namna ya kutumia kazi au sanaa za kiutamaduni:

(a) matumizi, matayarisho ya nakala na kusambaza nakala za kazi za mambo ya utamaduni
(b) kuziwasilisha kwa umma ikijumuisha kuzicheza, kuzitangaza na kuzinukuu kazi hizo.

Kifungu 26: Kibali cha matumizi ya kazi za utamaduni hakihitajiki iwapo matumizi ni:

(i) kwa ajili ya kufundishia
(ii) kwa kunukuu
(iii) kuzitumia kwa ajili ya kutengeneza kazi ya jadi
(v) matumizi ya muda tu kwa kutoa taarifa

**BASATA**

Maombi kwa kibali cha/na masharti ya kibali cha BASATA yameelezwa vifungu 28 – 30.

**Sehemu IV: Masharti ya Hakishiriki za Wachezaji Waigizaji, Waimbaji, Wachapaji, Wachapishaji, Watengenezaji wa Kanda, Watangazaji n.k. (Vifungu 31 – 35)**

Kutokana na vipengele vya kifungu 5 cha sheria hii (inayohusu ulinzi wa hakimiliki, msanii (*performer*) atakuwa na haki kamili ya kufanya au kuruhusu wengine wafanye yafuatayo:

(a) kutangaza redioni/katika televisheni kazi zake
(b) kurekodi kazi zake kwenye kanda na filamu
(c) kutengeneza nakala za kanda na filamu zenye kazi zake
(d) kuuza kanda na filamu hizo
(e) kukodisha kanda na filamu zake
(f) kuwezesha umma upate matangazo yatokanayo na kazi zake zilizorekodiwa kwenye kanda/filamu.

Kifungu: 31(2) kinasema iwapo msanii ataruhusu kazi yake irekodiwe kwenye filamu haki za kiuchumi zilizotajwa hapo juu hazitatumika tena.

Kifungu: 31(3) kinampa msanii haki ya maadili kama zile za hakimiliki.

**Muda wa Ulinzi wa Hakishiriki**

Kifungu 31(5): hakishiriki italindwa kwa muda wa miaka 50 tangu kazi ilipotendwa au kanda iliporekodiwa.

**Haki za Kiuchumi za Mtengenezaji Kanda – Muziki, Michezo n.k.**

Kifungu 32(1): Kutokana na vipengele vya kifungu 5 (hakimiliki) mtengenezaji wa kanda hizo ana haki kamili za:

(a) kutengeneza nakala za kanda hizo
(b) kuwezesha umma upate kanda hizo, kwa mauzo
(c) kuzikodisha kanda
(d) kuwezesha umma upate matangazo ya kazi zake zilizorekodiwa kwenye kanda.

**Muda wa Ulinzi wa Kanda**

Hadi mwisho wa mwaka wa 50 tangu uchapishaji – Kifungu 32(2).

**Malipo kwa Utumiaji wa Kanda za Sauti**

Iwapo matangazo yatafanyika katika vyombo kwa redio na televisheni kutoka kazi iliyorekodiwa kwenye kanda mtumiaji atawalipa, pamoja, msanii (au wasanii) na mtayarishaji wa kanda – Kifungu 33(1). Mtayarishaji wa kanda atamlipa msanii (wasanii) nusu ya fedha alizolipwa na mtumiaji kifungu 33(2).

**Haki za Kiuchumi za Vyombo vya Matangazo (ya Redio/Televisheni)**
Kifungu 34(1)

Kutokana na vipengele vya kifungu cha 5 (Hakimiliki) vyombo vya habari vitakuwa na haki kamili ya kufanya au kuruhusu wengine wafanye yafuatayo:-

(a) kutangaza upya matangazo yake
(b) kuwasilisha kwa umma matangazo yake
(c) kurekodi kwenye kanda matangazo yake
(d) kutengeneza nakala za kanda hizo.

**Muda wa Ulinzi wa Matangazo**

Kifungu 34(2): Ulinzi unadumu hadi mwisho wa mwaka wa 50 tangu tangazo litolewe.

**Mabano ya Hakimiliki za Wasanii Chini ya Vifungu 31 – 34**

Kifungu 35 kinachanganua kazi za wasanii ambazo hazihitaji kibali cha msanii ili kuzitumia. Vifungu hivyo havitatumika katika matendo yanayokatazwa iwapo sehemu za kazi hizo zitatumika kwa kutoa taarifa ya habari, kufanyia utafiti, kufundishia n.k.

**Sehemu V: Makosa ya Ukiukwaji na Adhabu**

Ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa:-

(a) Aya ya 41 ya *The Trade Related Aspects of Intellectual Property Right* (Makubaliano ya *TRIPS*) – nchi wanachama kutunga sheria na kanuni kali – na Aya ya 61 – kutoa adhabu kali kwa ukiukaji wa makusudi wa hakimiliki na hakishiriki.
(b) Aya ya 14 ya *WIPO Copyright Treaty*
(c) Aya ya 23 ya *WIPO Performances and phonograms Treaty.*

Sehemu hii inasisitiza kuwa haki za wasanii zinalindwa na wakiukaji wanaadhibiwa vikali.

**Marekebisho ya Madai**

Kifungu 36(1): Msanii yeyote ambaye haki yake iko katika hatari ya/au tayari imekiukwa anaweza kuomba mahakama ya Wilaya itoe amri ya:

(a) kizuizi
(b) malipo ya fidia, faida iliyopatikana na gharama.

Kifungu 36(2): Chochote kinachohusika na utayarishaji wa ukiukwaji kikamatwe.

Kifungu 38(1): Nakala za vifaa vinavyokiuka haki ziharibiwe.

Kifungu 39: Nakala za vitu vinavyokiuka haki vikabidhiwe kwa msanii ili aviuze.

Kifungu 40: Mwenye kampuni inayofanya ukiukaji atawajibika kikamilifu kwa vitendo vya wafanyakazi wake.

Kifungu 41: Iwapo ukiukwaji haukuwa wa makusudi mkiukaji atamlipa msanii fedha za kufidia hasara tu iliyopatikana.

**Makosa ya Jinai na Adhabu**

Kifungu 42(1) –(9):- licha ya marekebisho ya madai chini ya kifungu 36, mtu yeyote ambaye kwa makusudi anakiuka haki za msanii atatozwa faini isiyozidi Shs. 5,000,000/= hadi Shs. 10,000,000/= na/au kupata kifungo kisichozidi miaka 3 – 5.

Kifungu 43(1)-(4): Sheria za:

*(a)* *The Civil Procedure Code, 1966*
*(b)* *The Criminal Procedure Act, 1985*
*(c)* *The Tanzania Revenue Act, 1995*

Zitatumika katika sheria hii isipokuwa kifungu 170(2) cha *The Criminal Procedure Act, 1995.*

**Sehemu VI: Ulinzi wa Kiteknolojia na Taarifa za Kutawala Haki**

Kifungu 44: Aya za 11 na 12 za *WIPO Copyright Treaty* na Aya za 18-19 za *WIPO Performances and Phonograms Treaty* zinashughulikia suala la ulinzi wa kiteknolojia na umuhimu wa kulinda taarifa (takwimu) zinazohusu utetezi wa haki hizo.

Kifungu 44(1): Vitendo vifuatavyo vinatambuliwa kama ukiukwaji wa hakimiliki/hakishiriki:

(a) utengenezaji au uingizaji nchini wa kifaa ambacho, kwa makusudi, kimetengenezwa ili kuzuia/ kupunguza utengenezaji wa nakala za kazi au kuharibu hadhi ya nakala;
(b) utengenezaji au uingizaji nchini wa kifaa ambacho kinaweza kunasa siri, kwa watu wasiolengwa kutumiwa programu;
(c) uondoaji wa taarifa zenye maelezo au takwimu kielektroniki za kutetea haki;
(d) usambazaji au utangazaji wa kazi, kanda na matangazo wakati takwimu za utetezi na haki zimeondolewa.

Kifungu 45: Waziri anayeshughulikia masuala ya hakimiliki na hakishiriki ana uwezo wa kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

**Chama cha Hakimiliki cha Tanzania (COSOTA)**

Kifungu 46: Chama cha Hakimiliki cha Tanzania kinaanzishwa kwa mujibu wa sheria.

Kifungu 47: Kinaelezea shughuli za COSOTA.

(a) kukuza na kulinda haki za wasanii, watunzi, watafsiri, watengenezaji wa kanda, watangazaji na hasa kukusanya na kuzigawa fedha zinazotokana na kazi zao.
(b) Kutunza regista za kazi na wasanii;
(c) Kutafuta, kutambua na kulinda haki za wasanii hao na kutoa ushahidi mahakamani n.k.;

(d) Kuchapisha vitabu, makala, taarifa juu ya 'hakimiliki na hakishiriki';

(e) Kumshauri Waziri.

Kifungu 48-9: vinashughulikia ada na fedha za chama.

Kifungu 51: (pamoja na Kiambatanisho): vinaelezea katiba, vikao na masuala mengine ya COSOTA.

**Sehemu VII: Vipengele vya Mpito**

Sheria hii inafuata sheria ya Hakimiliki ya mwaka 1966 na kazi za sanaa zilizokuwepo kabla ya sheria hii zinalindwa iwapo muda wa ulinzi chini ya sheria ya 1966 haujamalizika.

Mwisho sheria hii italinda mikataba ya wasanii iliyokuwepo kabla ya sheria hii.